

Maji ni mojawapo ya maliasili tuliyopewa na Mungu. Maji yana umuhimu gani? Bila shaka unafamu kuwa hatuwezi tukatekeleza shughuli nyingi za nyumbani bila maji. Usafi wa mwili na mazingira huhitaji maji. Upishi nao hauwezi ukafanyika ipasavyo pasi na maji. Katika zaraa, maji hutumika kunyunyizia mimea na kuchanganyia kemikali za kuwaua wadudu waharibifu. Je, unajua matumizi gani mengine ya maji?

Miti nayo ina faida chungu nzima. Miti mingi iwapo pamoja huunda msitu. Misitu ni makao ya wanyamapori na viumbe wengine kama vile ndege wa porini. Katika misitu, hupatikana chakula cha wanyama na binadamu. Aidha, kuna dawa za kienyeji ambazo hupatikana kutokana na miti hiyo iliyo misituni. Faida nyingine ya misitu ni kuvutia mvua, kurembesha mandhari na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Tujitolee mhanga kutunza misitu, mito, maziwa na bahari.